

TARGETER WINGS
KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI
GREDI 4 - 2022
KISWAHILI LUGHA



Muda: Saa 1

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1-5



- Rehema :** Hujambo Yohana?
Yohana : Sijambo Rehema.Habari za utokako?
Rehema : Salama. Na unaenda wapi?
Yohana : Naenda dukani kununua mkate.
Rehema : Mbona unaenda peke yako?
Je, mko wangapi kwenu?
Yohana : Tuko watoto watano. Mimi ni kitindamimba.
Rehema : Mimi ni mwanambee kwa familia ya watoto wanne. Kwaheri.
Yohana : Kwaheri ya kuonana.

1. Kulingana na kifungu, wahusika ni wangapi?
A. Wawili
B. Wanne
C. Mmoja
D. Wataatu
2. Tambua maagano yaliyotumiwa katika kifungu hiki?
A. Sijambo
B. Hodi
C. Alamsiki
D. Kitindamimba

TW - 006

1

KISWAHILI GREDI 4

3. Neno lipi ni kinyume cha kitindamimba?

A. Kifunguamimba	B. Ndugu
C. Mnuna	D. Mziwanda
4. Yohana alikuwa anaelekea wapi?

A. Sokoni	B. Dukani
C. Nyumbani	D. Mjini
5. Eleza maana ya neno **mwanaambee**.
 - A. Mwana wa kwanza katika familia
 - B. Mwana wa pili katika familia
 - C. Mwana wa mwisho katika familia
 - D. Mwana wa tatu katika familia

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali 6-10

Siku moja jioni, watoto waliokuwa wametoka katika mashindano ya michezo walifika hapo. Walifika wakiwa wamechoka sana. Waliamua kuketi kwenye nyasi zile ili kupumzika na kula matunda waliyokuwa wamebeba. Walikuwa na maembe, ndizi, mapapai na mafenesi.

Watoto waliyaosha matunda yao kwa maji waliyokuwa wamebeba kwenye chupa zao. Walipomaliza kula walitupa mbegu za matunda kwenye udongo. Baada ya miaka mingi mbegu zilimea na kuwa miti mikubwa.

6. Kwa nini watoto waliketi kwenye nyasi?

A. Walikuwa wametoka katika mashindano	B. Ili wale wali
C. Waliamua kucheza hapo	D. Ili wapumzike
7. Watoto walikuwa na matunda haya yote isipokuwa _____.

A. maparachichi	B. mapapai
C. ndizi	D. maembe
8. Watoto hao walikuwa wametoka wapi?

A. Kuchota maji	B. Mashindanoni
C. Kula matunda	D. Kupanda mbegu
9. Watoto hao walikuwa wamebeba maji wapi?

A. Kwenye ndoo	B. Kwenye mitungi
C. Kwenye chupa	D. Kwenye pipa
10. Baada ya kula matunda, watoto hao walifanya nini?
 - A. Walienda shuleni
 - B. Walienda shambani
 - C. Walienda kuteka maji
 - D. Walitupa mbegu za matunda kwenye udongo

Soma kifungu hiki kisha ujaze mapengo 11-15

Dakika chache, baada ya saa **11** asubuhi, wazazi walianza kumiminika shuleni. Walionekana wenye furaha na hamu ya kujua maendeleo ya wana **12** shuleni. Wengine waliingia shuleni **13** magari yao ya kifahari yaliyotuacha na bumbuazi. Kuna wale ambao walitembea kwa vile **14** na magari. Mzazi ambaye alitufurahisha **15** wote ni yule aliyefika akiwa amebebwa na tuktuk iliyopambwa ikapambika.

- | | | | | |
|-----|-------------|-------------|-------------|-------------|
| 11. | A. ya pili | B. wawili | C. mbili | D. mawili |
| 12. | A. wenu | B. yao | C. wao | D. zao |
| 13. | A. pamoja | B. ndani | C. kwa | D. kwenye |
| 14. | A. hawakuua | B. hawakuwa | C. hakuwa. | D. hawakua |
| 15. | A. kuniliko | B. kuliko | C. kuwaliko | D. kutuliko |

Kuanzia nambari 16-30, jibu swali kulingana na maagizo.

16. Ni neno lipi lisilo la heshima?
A. Naomba B. Tafadhali
C. Nataka D. Kunradhi
17. Neno **jino** linapatikana katika ngeli gani?
A. I - I B. I - ZI
C. LI - YA D. YA -YA
18. Andika sentensi hii kwa wakati ujao
Jambazi alikamatwa njiani.
A. Jambazi amekamatwa njiani.
B. Jambazi atakamatwa njiani.
C. Jambazi hukamatwa njiani.
D. Jambazi anakamatwa njiani.
19. Kamilisha tashbihi hii.
Mwembamba kama _____
A. fuko B. nguruwe
C. sindano D. nyundo
20. Andika sentensi hii kwa wingi
Mwalimu alinifundisha vizuri
A. Walimu walitufundisha vizuri.
B. Walimu walinifundisha vizuri.
C. Mwalimu alitufundisha vizuri.
D. Mwalimu aliwafundishi vizuri.

21. Tegua kitendawili hiki: **Huku ng'o na kule ng'o.**
 A. Giza B. Hindi
 C. Usingizi D. Yai
22. Kanusha sentensi:
Miti michanga itapaliliwa.
 A. Miti michanga hautapaliliwa.
 B. Miti michanga haijapaliliwa
 C. Miti michanga haitapaliliwa
 D. Miti michanga haipaliliwi
23. Andika kitenzi hiki kiwe katika kauli ya kutendwa
Kata
 A. Katiwa B. Katwa
 C. Katika D. Katisha
24. Tambua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo
Mimi ni mwanafunzi mzuri.
 A. mwanafunzi B. ni
 C. mzuri D. mimi
25. Neno gani ni nomino kati ya haya?
 A. Jenga B. Mlima
 C. Soma D. Lala
26. Dada wa babangu nitamuita _
 A. shangazi B. shemeji
 C. halati D. binamu
27. Tumia kiulizi 'ngapi' kwa usahihi. Funguo _____ zimeshika kutu?
 A. ngapi B. vingapi
 C. mingapi D. mangapi
28. Kamilisha methali: **Mtoto umleavyo.**
 A. siku ya ngoma B. ndivyo akuavyo
 C. huvunjika guu D. angali mdogo
29. Udogo wa neno 'mti' ni
 A. jiti B. vijiti
 C. kijiti D. kiti
30. Chumba katika nyumba kinachotumika kwa kupokelea wageni huitwaje?
 A. Sebule B. Jikoni
 C. Roshani D. Bafu